

Neno la Alhamisi, 31. Julai 2014

Miisho yote ya dunia itakumbuka
na kumgeukia BWANA jamaa zote
za mataifa watasujudu mbele zake.
Zaburi 22,27

Yesu akasema:
Sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi.
Mathayo 9,13

All the ends of the earth shall remember and turn to the Lord,
and all the families of the nations shall worship before you.

Psalm 22:27 (ESV)

Jesus said:
I came not to call the righteous, but sinners.
Matthew 9:13 (ESV)

Neno Julai 2014 The Word July 2014

Kiswahili Contemporary Version 2006
English Standard Version



Project Bible 2.0 www.bible2.net

Neno la Jumanne, 29. Julai 2014

Abramu alipokuwa na miaka tisini na tisa,
BWANA akamtokea akamwambia,
“Mimi ndimi Mungu Mwenye Nguvu,
enenda mbele zangu na uishi kwa unyofu.
Mwanzo 17,1

Kwa hiyo, kwa kuwa tunapokea ufalme
ule ambaao hauwezi kutetemeshwa,
basi na tuwe na shukrani na
hivyo tumwabudu Mungu kwa namna inavyompendeza,
kwa unyenyekevu na uchaji.
Waeranania 12,28

I am God Almighty;
walk before me, and be blameless.
Genesis 17:1 (ESV)

Let us be grateful
for receiving a kingdom that cannot be shaken,
and thus let us offer to God acceptable worship,
with reverence and awe.
Hebrews 12:28 (ESV)

Neno la Jumatano, 2. Julai 2014

Tunapotumaini kupata kitu ambacho hatuna,
basi twakingojea kwa saburi.
Warumi 8,25

Msilitupe tumaini lenu,
kwa maana lina thawabu kubwa mno.
Inawapasa kuvumilia ili mkiisha
kufanya mapenzi ya Mungu mpate kile alichoahidi.
Waeranania 10,35-36

If we hope for what we do not see,
we wait for it with patience.
Romans 8:25 (ESV)

Do not throw away your confidence,
which has a great reward.
For you have need of endurance,
so that when you have done the will of God
you may receive what is promised.
Hebrews 10:35-36 (ESV)

Neno la Jumapili, 27. Julai 2014

Fanya lililo haki na jema mbele
za BWANA ili upate kufanikiwa,
uweze kuingia na kuimiliki nchi nzuri
ambayo BWANA aliahidi kwa kiapo kwa baba zako.

Kumbukumbu La Torati 6,18

Kamba za mpaka zimeniangukia mahali pazuri,
hakika nimepata urithi mzuri.

Zaburi 16,6

You shall do what is right and good in the sight of the Lord,
that it may go well with you,
and that you may go in and take possession of the good land
that the Lord swore to give to your fathers.

Deuteronomy 6:18 (ESV)

The lines have fallen for me in pleasant places;
indeed, I have a beautiful inheritance.

Psalm 16:6

Neno la Ijumaa, 4. Julai 2014

Walipokuwa njiani wakienda,
mtu mmoja akamwambia Yesu,
"Nitakufuata kokote uendako."

Luka 9,57

Ee Mungu,
nichunguze, uujue moyo wangu,
nijaribu na ujue mawazo yangu.

Uone kama kuna njia iletayo machukizo ndani yangu,
uniongoze katika njia ya milele.

Zaburi 139,23-24

As they were going along the road,
someone said to Jesus,
I will follow you wherever you go.
Luke 9:57 (ESV)

Search me, O God, and know my heart!
Try me and know my thoughts!
And see if there be any grievous way in me,
and lead me in the way everlasting!
Psalm 139:23-24 (ESV)

Neno la Ijumaa, 25. Julai 2014

Waliimba nyimbo za sifa na za shukrani kwa BWANA hivi:
"Yeye ni mwema,
upendo wake kwa Israeli wadumu milele."
Ezra 3,11

Furahini katika Bwana sikuzote, tena nasema furahini!
Wafilipi 4,4

They sang responsively,
praising and giving thanks to the Lord,
"For he is good, for his steadfast love
endures forever toward Israel."
Ezra 3:11 (ESV)

Rejoice in the Lord always;
again I will say, Rejoice.
Philippians 4:4 (ESV)

Neno la Jumapili, 6. Julai 2014

kwa maana yeye humtosheleza
mwenye kiu na kumshibisha mwenye njaa kwa vitu vyema.
Zaburi 107,9

Yesu akawaambia, "Hakuna sababu ya wao kuondoka.
Ninyi wapeni chakula."
Mathayo 14,16

The Lord satisfies the longing soul,
and the hungry soul he fills with good things.
Psalm 107:9 (ESV)

Jesus said to the disciples:
They need not go away;
you give them something to eat.
Matthew 14:16 (ESV)

Neno la Jumatano, 23. Julai 2014

Ee BWANA, uwe na huruma! Utakawia hata lini?
Wahurumie watumishi wako.
Zaburi 90,13

BWANA atahukumu watu wake
na kuwahurumia watumishi wake
anapoona nguvu zao zimekwisha wala
hakuna ye yote aliyebak,
mtumwa au aliye huru.
Kumbukumbu La Torati 32,36

Return, O Lord! How long?
Have pity on your servants!
Psalm 90:13 (ESV)

The Lord will vindicate his people
and have compassion on his servants.
Deuteronomy 32:36 (ESV)

Neno la Jumatatu, 21. Julai 2014

Tumwogope BWANA Mungu wetu,
anayetupatia mvua za masika na za vuli kwa majira yake,
anayetuhakikishia majuma ya mavuno kwa utaratibu.
Yeremia 5,24

Mungu hakuacha kuwaonyesha watu uwepo wake:
Ameonyesha wema kwa kuwanyeshea
mvua toka mbinguni na kuwapa mazao kwa majira yake,
naye amewapatia chakula tele
na kuijaza miyo yenu na furaha.
Matendo ya Mitume 14,17

Let us fear the Lord our God,
who gives the rain in its season,
the autumn rain and the spring rain,
and keeps for us the weeks appointed for the harvest.
Jeremiah 5:24 (ESV)

God did not leave himself without witness,
for he did good by giving you
rains from heaven and fruitful seasons,
satisfying your hearts with food and gladness.
Acts 14:17 (ESV)

Neno la Jumanne, 8. Julai 2014

Nimeishi muda mrefu mno mionganii mwa wale
wanaochukia amani.
Mimi ni mtu wa amani, lakini ninaposema,
wao wanataka vita.
Zaburi 120,6-7

Taifa halitainua upanga dhidi ya taifa jingine,
wala hayatafanya mazoezi ya vita tena.
Isaya 2,4

Too long have I had my dwelling
among those who hate peace.
I am for peace,
but when I speak, they are for war!
Psalm 120:6-7 (ESV)

Nation shall not lift up sword against nation,
neither shall they learn war anymore.
Isaiah 2:4

Neno la Alhamisi, 10. Julai 2014

Nitakuwa na rehema kwake yeye nimrehemuye,
pia nitakuwa na huruma kwake yeye nimhurumiaye.
Kutoka 33,19

Je, sina haki yangu kufanya kile nitakacho
na mali yangu mwenyewe?
Au unaona vivu kwa kuwa nimekuwa mkarimu?
Mathayo 20,15

I will be gracious to whom I will be gracious,
and will show mercy on whom I will show mercy.
Exodus 33:19 (ESV)

In the parable the vineyard said to a grumbling laborer:
Am I not allowed to do what I choose
with what belongs to me?
Or do you begrudge my generosity?
Matthew 20:15

Neno la Jumamosi, 19. Julai 2014

Ongoza hatua zangu kulingana na neno lako,
usiache dhambi ye yote initawale.
Zaburi 119,133

Kesheni, simameni imara katika imani,
iweni mashujaa na hodari.
1 Wakorinto 16,13

Keep steady my steps according to your promise,
and let no iniquity get dominion over me.

Psalm 119:133 (ESV)

Be watchful, stand firm in the faith,
act like men, be strong.
1 Corinthians 16:13 (ESV)

Neno la Jumamosi, 12. Julai 2014

Yeye aliyetumwa na Mungu husema maneno ya Mungu,
kwa kuwa Mungu humtoa Roho pasipo kipimo.
Yohana 3,34

BWANA Mwenyezi amenipa ulimi uliofundishwa,
ili kujua neno lile limtegomezalo aliyechoka.
Isaya 50,4

He whom God has sent utters the words of God,
for he gives the Spirit without measure.

John 3:34 (ESV)

The Lord God has given me
the tongue of those who are taught,
that I may know how to sustain with a word
him who is weary.
Isaiah 50:4 (ESV)

Neno la Alhamisi, 17. Julai 2014

BWANA atatawala milele na milele.
Kutoka 15,18

Ufalme wa ulimwengu umekuwa
ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake,
naye atatawala milele na milele.
Ufunuo wa Yohana 11,15

The Lord will reign forever and ever.
Exodus 15:18 (ESV)

The kingdom of the world has become
the kingdom of our Lord and of his Christ,
and he shall reign forever and ever.

Revelation 11:15 (ESV)

Neno la Jumatatu, 14. Julai 2014

Abramu akamwamini BWANA, naye kwake hili
likahesabiwa kuwa haki.
Mwanzo 15,6

Mungu alikuwa ndani ya Kristo
akiupatanisha ulimwengu na nafsi Yake mwenywewe,
akiwa hawahesabii watu dhambi zao. Naye
ametukabidhi sisi ujumbe huu wa upatanisho.
2 Wakorinto 5,19

Abram believed the Lord,
and he counted it to him as righteousness.
Genesis 15:6 (ESV)

In Christ God was reconciling the world to himself,
not counting their trespasses against them,
and entrusting to us the message of reconciliation.

2 Corinthians 5:19 (ESV)

Neno la Jumanne, 1. Julai 2014

Msidanganyike,
"Ushirika na watu wabaya huharibu tabia njema."
Zindukeni mwe na akili kama iwapasavyo,
msitende dhambi tena, kwa maana watu wengine
hawamjui Mungu.
Nasema mambo haya ili mwone aibu.
1 Wakorinto 15,33-34

Mwisho wa mambo yote umekaribia.
Kwa hiyo iweni na akili pia mwe na kiasi mkikesha katika
kuomba.
1 Petro 4,7

Do not be deceived:
"Bad company ruins good morals."
Wake up from your drunken stupor, as is right,
and do not go on sinning.
For some have no knowledge of God.
I say this to your shame.
1 Corinthians 15:33-34 (ESV)

The end of all things is at hand;
therefore be self-controlled and sober-minded
for the sake of your prayers.
1 Peter 4:7 (ESV)

Neno la Alhamisi, 3. Julai 2014

Pia Seti akamzaa mwana akamwita Enoshi.
Wakati huo watu wakaanza kuliitia jina la BWANA.
Mwanzo 4,26

Lakini ye yote atakayeliita jina la Bwana, ataokolewa.
Matendo ya Mitume 2,21

At the time of Adam's son Seth:
At that time people began to call upon the name of the Lord.
Genesis 4:26

Everyone who calls upon the name of the Lord shall be saved.
Acts 2:21 (ESV)

Taken from The Holy Bible, English Standard Version 
copyright (c) 2001 by Crossway Bibles,
a division of Good News Publishers.
Used by permission. All rights reserved.

Neno la Jumatano, 30. Julai 2014

Kama baba alivyo na huruma kwa watoto wake,
ndivyo BWANA anavyowahurumia wale wanaomcha.
Zaburi 103,13

Ikiwa Mungu anayavika hivi majani ya shambani,
ambayo leo yapo na kesho yanatupwa motoni,
je, hatawavika ninyi vizuri zaidi, enyi wa imani haba?
Mathayo 6,30

As a father shows compassion to his children,
so the Lord shows compassion to those who fear him.
Psalm 103:13 (ESV)

If God so clothes the grass of the field,
which today is alive and tomorrow is thrown into the oven,
will he not much more clothe you, O you of little faith?
Matthew 6:30 (ESV)

Neno la Jumatatu, 28. Julai 2014

Yule atakayevumilia hadi mwisho ndiye atakayeokoka.
Mathayo 24,13

Je, hamjui kwamba katika mashindano
ya mbio wote wanaoshindana hukimbia,
lakini ni mmoja wao tu apewaye tuzo?
Kwa hiyo kimbieni katika mashindano
kwa jinsi ambavyo mtapata tuzo.
1 Wakorinto 9,24

The one who endures to the end will be saved.
Matthew 24:13 (ESV)

Do you not know that in a race all the runners run,
but only one receives the prize?
So run that you may obtain it.
1 Corinthians 9:24 (ESV)

Neno la Jumamosi, 5. Julai 2014

Maskini wataona na kufurahi,
ninyi mnaomtafuta Mungu, miyo yenu na iishi!
Zaburi 69,32

Alinileta nje mahali penye nafasi tele,
akaniokoa kwa kuwa alipendezwa nami.
Zaburi 18,19

You who seek God, let your hearts revive.
Psalm 69:32 (ESV)

He brought me out into a broad place;
he rescued me, because he delighted in me.
Psalm 18:19 (ESV)

Neno la Jumatatu, 7. Julai 2014

Wakakataa kusikiliza na kushindwa
kukumbuka miujiza ulioifanya mionganii mwao.
Wakawa na shingo ngumu na katika
uasi wao wakamchagua kiongozi ili warudi
kwenye utumwa wao.

Lakini weweni Mungu mwenye kusamehe,
mwenye neema na mwangi wa huruma,
si mwelesi wa hasira, ni mwangi wa upendo.

Kwa hiyohukuwaacha,

Nehemia 9,17

Bwana hakawii kuitimiza ahadi
Yake kama watu wengine wanavyodhani kukawia,
bali Yeye anawavumilia,
maana hataki mtu ye yote aangamie,
bali kila mmoja afikilie toba.
2 Petro 3,9

You are a God ready to forgive,
gracious and merciful,
slow to anger and abounding in steadfast love.
Nehemiah 9:17

The Lord is not slow to fulfill his promise
as some count slowness,
but is patient toward you,
not wishing that any should perish,
but that all should reach repentance.
2 Peter 3:9

Neno la Jumamosi, 26. Julai 2014

Huwainua juu wanyonge,
nao wale waombolezao
huinuliwa wakawa salama.
Ayubu 5,11

Wana heri wale wanaohuzunika, maana hao watafarijiwa.
Mathayo 5,4

God sets on high those who are lowly,
and those who mourn are lifted to safety.
Job 5:11 (ESV)

Blessed are those who mourn,
for they shall be comforted.
Matthew 5:4 (ESV)

Neno la Alhamisi, 24. Julai 2014

Kutoka katika vilindi ninakulilia,
Ee BWANA, Ee BWANA, sikia sauti yangu.
Zaburi 130,1-2

Nilizama chini sana mpaka pande za mwisho za milima,
makomeo ya hiyo nchi yalinifungia hata milele.
Lakini uliuleta uhai wangu kutoka shimonii,
Ee BWANA Mungu wangu.
Yona 2,6

Out of the depths I cry to you, O Lord!
O Lord, hear my voice!
Psalm 130:1-2 (ESV)

You brought up my life from the pit,
O Lord my God.
Jonah 2:6

Neno la Jumatano, 9. Julai 2014

Nihifadhi sawasawa na ahadi yako,
nami nitaishi, usiache matumaini yangu yakavunjwa.
Zaburi 119,116

Fuata haki, utauwa, imani, upendo, saburi na upole.
1 Timotheo 6,11

Uphold me according to your promise, that I may live,
and let me not be put to shame in my hope!

Psalm 119:116 (ESV)

Pursue righteousness, godliness, faith,
love, steadfastness, gentleness.

1 Timothy 6:11 (ESV)

*Uphold me according to your promise, that I may live,
and let me not be put to shame in my hope!*

Neno la Jumanne, 22. Julai 2014

Lakini yalikuwa ni mapenzi
ya BWANA kumchubua na kumsababisha ateseke,
ingawa BWANA amefanya maisha
yake kuwa sadaka ya hatia,
ataona uzao wake na kuishi siku nyingi,
nayo mapenzi ya BWANA yatafanikiwa mkononi mwake.
Isaya 53,10

Kwa kuwa ninyi mliitwa kwa ajili ya hayo,
kwa sababu Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu,
akiwaachia kielelezo, ili mzifuate nyayo zake.
1 Petro 2,21

When his soul makes an offering for guilt,
he shall see his offspring; he shall prolong his days;
the will of the Lord shall prosper in his hand.

Isaiah 53:10

Peter writes about suffering when doing good:

To this you have been called,
because Christ also suffered for you,
leaving you an example,
so that you might follow in his steps.

1 Peter 2:21 (ESV)

Neno la Ijumaa, 11. Julai 2014

Mnajisumbua bure kuamka mapema na kuchelewa kulala,
mkitaabikia chakula,
kwa maana ye ye huwapa usingizi wapenzi wake.
Zaburi 127,2

Ahimidiwe Mungu na Baba wa Bwana wetu
Yesu Kristo aliyetubariki sisi kwa baraka zote za rohoni,
katika ulimwengu wa roho ndani ya Kristo.
Waefeso 1,3

It is in vain that you rise up early
and go late to rest,
eating the bread of anxious toil;
for he gives to his beloved sleep.

Psalm 127:2 (ESV)

Blessed be the God and Father of our Lord Jesus Christ,
who has blessed us in Christ
with every spiritual blessing in the heavenly places.

Ephesians 1:3 (ESV)

Neno la Jumapili, 20. Julai 2014

Lakini Noa akapata kibali machoni pa BWANA.
Mwanzo 6,8

Kwa maana neema ya Mungu
iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa.
Tito 2,11

Noah found favor in the eyes of the Lord.
Genesis 6:8 (ESV)

The grace of God has appeared,
bringing salvation for all people.
Titus 2:11 (ESV)



Neno la Jumapili, 13. Julai 2014

Mungu wa mbinguni atatufanikisha.
Sisi watumishi wake tutaanza kujenga tena.
Nehemia 2,20

Lakini hamjui hata litakalotukia kesho. Maisha yenu ni nini?
Ninyi ni ukungu ambaa huonekana
kwa kitambo kidogo kisha hutoweka.
Badala yake, inawapasa kusema,
"Kama Bwana akipenda, tutaishi na kufanya hili ama lile."
Yakobo 4,14-15

The God of heaven will make us prosper,
and we his servants will arise and build.
Nehemiah 2:20 (ESV)

You do not know what tomorrow will bring.
What is your life? For you are a mist
that appears for a little time and then vanishes.
Instead you ought to say,
If the Lord wills, we will live and do this or that.
James 4:14-15

Neno la Jumanne, 15. Julai 2014

Mna heri ninyi watu watakapowashutumu
na kuwatesa na kunena dhidi
yenu mabaya ya aina zote kwa uongo kwa ajili yangu.
Furahini na kushangilia kwa maana thawabu yenu ni kuu.
Mathayo 5,11-12

Ninakuja upesi.
Shika sana ulicho nacho, ili mtu asije akaichukua taji yako.
Ufunuo wa Yohana 3,11

Blessed are you
when others revile you and persecute you
and utter all kinds of evil against you
falsely on my account.
Rejoice and be glad,
for your reward is great in heaven.
Matthew 5:11-12 (ESV)

I am coming soon.
Hold fast what you have,
so that no one may seize your crown.
Revelation 3:11

Neno la Ijumaa, 18. Julai 2014

Mwanamume na mkewe,
wakajificha kutoka mbele za
BWANA Mungu.
Mwanzo 3,8

Hakuna kilichofichika ambacho hakitafunuliwa,
wala hakuna jambo lo lote la siri ambalo halitaletwa nuruni.
Marko 4,22

The man and his wife hid themselves
from the presence of the Lord God.
Genesis 3:8 (ESV)

Nothing is hidden except to be made manifest;
nor is anything secret except to come to light.
Mark 4:22 (ESV)

Neno la Jumatano, 16. Julai 2014

Hakuna mtu ye yote awezaye
kuwatumikia mabwana wawili,
kwa kuwa ama atamchukia huyu
na kumpenda yule mwingine,
au atashikamana sana na huyu
na kumdharaau huyu mwingine.
Ninyi hamwezi kumtumikia Mungu na mali.
Mathayo 6,24

Je, hamjui kwamba mnapojoitoa kwa
mtu ye yote kama watumwa watifu,
ninyi ni watumwa wa yule mnayemtii,
aidha watumwa wa dhambi,
ambayo matokeo yake ni mauti,
au wa utii ambaao matokeo yake ni haki?
Warumi 6,16

No one can serve two masters,
for either he will hate the one and love the other,
or he will be devoted to the one and despise the other.
You cannot serve God and money.
Matthew 6:24 (ESV)

Do you not know that
if you present yourselves to anyone as obedient slaves,
you are slaves of the one whom you obey,
either of sin, which leads to death,
or of obedience, which leads to righteousness?
Romans 6:16 (ESV)